AFRIPRISE
INVESTMENT PLC.

TANGAZO

LA MKUTANO MKUU WA 21 WA MWAKA WA WANAHISA

Tunayo furaha kuwataarifu kwamba Mkutano Mkuu wa 21 wa Mwaka wa Wanahisa wa **AFRIPRISE INVESTMENT PLC** utafanyika kwa njia ya mtandao siku ya Jumamosi, tarehe 21 Novemba 2026, kuanzia saa 3:00 asubuhi. Kampuni itawapatia wanahisa wote taarifa za kuingia kwenye mkutano na maelekezo ya jinsi ya kujiunga na kushiriki kidijitali kupitia simu zao za mkononi.

AJENDA YA MKUTANO MKUU WA 21 WA MWAKA NI KAMA IFUATAVYO:

1. Kufungua Mkutano Mkuu wa 21 wa Mwaka;
2. Kupokea na kuidhinisha ajenda ya Mkutano Mkuu wa 21 wa Mwaka;
3. Kuthibitisha kumbukumbu za Mkutano Mkuu wa 20 wa Mwaka;
4. Kujadili masuala yaliyojitokeza kutokana na Mkutano Mkuu wa 20 wa Mwaka;
5. Kupokea, kujadili na kuidhinisha:
   a. Taarifa ya Mwenyekiti;
   b. Taarifa ya Afisa Mtendaji Mkuu;
   c. Taarifa ya Wakurugenzi na Taarifa za Fedha zilizokaguliwa kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 31 Desemba 2025;
6. Kupokea, kujadili na kuidhinisha pendekezo la Bodi kuhusu gawio la mwaka 2025;
7. Kupokea, kujadili na kuidhinisha pendekezo la Bodi kuhusu uteuzi wa Mkaguzi wa Hesabu wa Nje kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 31 Desemba 2026;
8. Kupokea, kujadili na kuidhinisha pendekezo kuhusu malipo ya wajumbe wa Bodi kwa mwaka 2026;
9. Kupokea na kujadili mapendekezo rasmi yaliyowasilishwa na wanahisa;
10. Kufunga Mkutano Mkuu wa 21 wa Mwaka.

TAARIFA MUHIMU:

1. **Mapendekezo kutoka kwa Wanahisa:** Wanahisa wanahimizwa kuwasilisha mapendekezo yao kwa maandishi kwa Katibu wa Kampuni kabla ya tarehe 10 Novemba 2026 ili yaingizwe katika kipengele namba 9 cha ajenda ya mkutano.
2. **Ripoti ya Mwaka na Nyaraka za Mkutano:** Ripoti ya Mwaka 2025 pamoja na nyaraka za mkutano zitapatikana kwenye tovuti ya Kampuni kuanzia tarehe 20 Oktoba 2026 kupitia: ***https://www.afriprise.co.tz.***
3. **Uwakilishi kwa Wakala:** Mwanahisa ambaye hataweza kuhudhuria mkutano anaombwa kumteua mwakilishi kwa kujaza Fomu ya Uwakilishi inayopatikana kwenye tovuti ya Kampuni www.afriprise.co.tz. Fomu zilizojazwa zitumwe kwa Katibu kupitia barua pepe ***info@afriprise.co.tz*** au ***WhatsApp namba 0757 138 048*** kabla ya tarehe 13 Novemba 2026, saa 4:00 usiku.
4. **Gawio:** Wakurugenzi wanapendekeza kulipa gawio la **TZS 23 kwa kila hisa.**
   – **Tarehe ya kutangazwa:** 01 Novemba 2026
   – **Hisa kuuzwa pamoja na haki ya gawio (cum-dividend):** 01 Novemba 2026
   – **Hisa kuuzwa bila haki ya gawio (ex-dividend):** kuanzia 19 Novemba 2026
   – **Tarehe ya kufunga rejista ya wanahisa:** 23 Novemba 2026
   – **Malipo ya gawio:** tarehe 30 Novemba 2026 au karibu na tarehe hiyo

Imetolewa kwa niaba ya Bodi ya Wakurugenzi.

Peter William Kifunguomali
Katibu wa Kampuni

AFRIPRISE INVESTMENT PLC
PSSSF Millenium Tower II, 24th Floor, Opposite Makumbusho Village, P. O. Box 72678, Dar es Salaam, Tanzania
Mobile: +255 753 701 802 | **Email:** info@afriprise.co.tz | **Website:** www.afriprise.co.tz